

LEKSIKOGRAFIA YA UUNDAJI KAMUSI NA KISWAHILI

UAMILIFU WA PICHA NA MICHORO KATIKA KAMUSI ZA KISWAHILI

Rachel Maina

Chuo Kikuu cha Mount Kenya

Ikisiri

Picha katika kamusi huwasilisha maana sawa na maneno. Japo leksikografia inahusu maneno, na hivyo hutumia maneno kuelezea maana, wakati mwingine inabidi kutumia mbinu mbadala ambazo zitafanya maana kueleweka vizuri zaidi. Picha na michoro hutumiwa kuonyesha wanyama, vitu au mimea ya kawaida, vitu ambavyo si rahisi kueleza kwa maneno kama vile maumbo, makundi ya vitu vinavyohusiana au maana ya kimsingi ya maneno ambayo kawaida hutumiwa kwa namna dhanifu au ya kitamathali. Ingawa kamusi za Kiswahili za awali hazikuwa na picha na michoro kwa wingi, zile ambazo zimechapishwa au kutolewa upya katika miaka ya hivi karibuni zinatumia picha na michoro kwa wingi kufafanua vitomeo mbalimbali. Makala hii inalenga kutathmini picha na michoro katika kamusi za Kiswahili na namna zinavyomfaa mtumiaji wa kamusi. Kamusi zitakazoangaziwa ni zile za kimapokeo, yaani zilizochapishwa, wala si za kidijitali.